# RIPOTI YA HAFLA YA KUAZIMISHA SIKU YA MTOTO WA AFRIKA ILIYOFANYIKA TAREHE 16 JUNI 2023 KATIKA VIWANJA VYA SHULE YA MSINGI CHAMAZI.

## UTANGULIZI

Hafla ya siku ya Mtoto wa Afrika, ilianza Kwa kuimba wimbo wa Taifa. Mwalimu Mkuu Shule ya Msingi Chamazi aliwakaribisha walimu waliohudhulia katika siku hiyo. Kisha Mkurugenzi wa shirika la ADOT aliwakaribisha wageni wote pamoja na timu ya utendaji kutoka shirika la ADOT.

Hafla ya Siku ya Mtoto wa Afrika ilifunguliwa rasmi mnamo saa 9:00 asubuhi. Historia fupi ya shirika la ADOT, maono ya shirika, malengo ya shirika pamoja na historia fupi ya Siku ya Mtoto wa Afrika yalitolewa katika salamu za utangulizi. Katika ufunguzi shirika la ADOT lilipongeza uongozi wa Shirika la Tanzania Human Right Defender Coalition (THRDC) Kwa msaada wa kiasi cha shillingi laki tatu na nusu za kitanzania (350,000/=) waliotoa kwa shirika la ADOT ambao umewawezesha kuwakutanisha kwa siku hiyo ya Mtoto wa Afrika tarehe 16 Juni 2023

## RISALA YA WATOTO WA SHULE YA MSINGI CHAMAZI KWENDA KWA MKURUGENZI WA SHIRIKA LA ADOT

Baada ya ufunguzi, ilisomwa risala kwenda Kwa Mkurugenzi wa shirika la ADOT huku wakiamini kuwa kupitia shirika hilo changamoto zao zitatatuliwa. Katika risala yao wamebainisha changamoto mbalimbali zinazowakumba watoto wenye ulemavu ikiwemo ukosefu wa viti mwendo kwa baadhi ya wanafunzi, umbali kufika shule na hali ngumu ya maisha katika maeneo wanayoishi. Risala hii imesomwa na Zaituni mtoto mwenye ulemavu wa viungo ambaye ni miongoni mwa wenye uhitaji wa viti mwendo.

*Mkurugenzi wa shirika la ADOT akiongea na  binti Zaituni,(darasa la sita) mtotomwenye ulemavu wa viungo asiyeweza kutembea kabisa.*

**WIMBO WA WATOTO WENYE ULEMAVU KWENDA MEZA KUU**

Mnamo saa 10:40 asubuhi, watoto wa Shule ya Msingi Chamazi na Msufini walijumuika kuonyesha vipaji vyao mbele ya meza kuu. Waliimba nyimbo mbalimbali za kusifia shirika kwa kuona thamani yao na kuacha shughuli zao na kujumuika nao shuleni hapo.

**RISALA YA WATOTO WA SHULE YA MSINGI MSUFINI KWA MGURUGENZI WA SHIRIKA LA ADOT**

Baada ya wimbo kumalizika, risala nyingine ilisomwa kwenda kwa Mkurugenzi wa Shirika la ADOT kutoka Shule ya Msingi Msufini. Katika risala yao waliweka bayana changamoto zinazowakumba watoto wenye ulemavu viziwi katika shule yao, ikiwemo uhaba wa walimu katika shule hiyo.

*Risala kutoka shule ya msingi Msufini iliyosomwa na binti Tahya*

**HOTUBA MAALUMU KUTOKA KWA MKURUGENZI WA SHIRIKA LA ADOT KWA WANAFUNZI WA SHULE YA MSINGI CHAMAZI NA MSUFINI.**

Mkurugenzi wa Shirika la ADOT alijibu risala za shule hizo mbili kwa kuchukua changamoto zinazowakumba watoto wenye ulemavu kwenye shule hizo na kuahidi kuwatafutia wafadhili zaidi ili aweze kutoa msaada kadiri ya maombi yao na ya wahitaji wengine nchini Tanzania kwa msaada wa Mungu na wadau wapenda maendeleo. Alisema "Kwasasa Shirika halina pesa, ila tutajitahidi kwa hali na mali kutafuta wafadhili ili tuweze kusaidia watoto wenye ulemavu Chamazi na Tanzania kwa ujumla".

*Mkurugenzi wa Shirika la ADOT akitoa risala yake mbele ya mgeni rasmi*

**IGIZO KUTOKA SHULE YA MSINGI MSUFINI**

Watoto wa Shule ya Msingi Msufini, waliigiza namna watoto wenye ulemavu wanavyopitia manyanyaso na mateso kuanzia wanapotoka nyumbani mpaka kufika shuleni. Pia walipendekeza suluhu ya changamoto zao ikiwemo kujengewa madarasa yenye miundombinu rafiki kwa watoto wenye ulemavu, kuongezewa walimu nk.

*Igizo la wanafunzi wa shule ya msingi Msufini Siku ya mtoto wa Afrika 2023.*

**RISALA MAALUM KUTOKA KWA MKURUGENZI WA SHIRIKA LA ADOT NDUGU ROSEMARY CHOMA KWENDA KWA MGENI RASMI MH. LAWRANCE GAMBA, DIWANI KATA YA CHAMAZI**

Mkurugenzi wa Shirika la ADOT alisoma risala mbele ya mgeni rasmi Mhe. Diwani wa Kata ya Chamazi ambapo alianza kwa kuushukuru uongozi wa Shirika la Tanzania Human Rights Defender Coalition (THRDC) kwa msaada wao wa Shilingi za Kitanzania Laki Tatu na Nusu (350,000/=) ambao ndio uliwawezesha kufanya maazimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika kwa mwaka 2023 na kukiri kwamba zilifanyika jitihada mbalimbali za kutafuta wafadhili kupitia mitandoa ya kijamii, baadhi ya mashirika na watu binafsi bila mafanikio. Kuwa kwenye hadhira hiyo siku ile kulimletea huzuni kwa upande mmoja kwa kuwa alijiona kuwa pendine hangeweza kuzitatua changamoto za watoto aliowaita yeye mwenyewe kwenye maadhimisho hayo lakini kwa upande mwingine alipata faraja kuona uwepo wa viongozi waliojitokeza siku hiyo akiwemo mgeni rasmi, Diwani wa Kata ya Chamazi ambaye aliaamini kuwa ataungana

naye katika kuzitatua changamoto za watoto hao na kutafuta wafadhili. Mkurugenzi pia aliwaasa watoto wote kuzingatia masomo na kutotumia vibaya utandawazi na/au matumizi mabaya ya simu ili kulinda utu na usalama wao.

*Mkurugenzi wa Shirika la ADOT, Rosemary Choma (kushoto) akitoa risala. Mhe. Diwani (kulia) akisikiliza kwa makini*

**HOTUBA YA MGENI RASMI MHE. DIWANI KWA MKURUGENZI WA SHIRIKA LA ADOT, WALIMU SHULE YA MSINGI CHAMAZI NA MSUFINI NA WAZAZI/WALEZI WANAOISHI NA WATOTO WENYE ULEMAVU.**

Mgeni rasmi alianza hotuba kwa kupongeza shirika la ADOT Kwa jitihana walizoonyesha kutafuta wadhamini wa kudhamini hafla ya Siku ya Mtoto wa Afrika. Kadhalika Mgeni rasmi

amewashukuru shirika la Tanzania Human Right Defender Coalition (THRDC) Kwa kutoa fedha zao kwa ajili ya kufadhili shughuli hiyo.

Mgeni rasmi alisema kwamba changamoto zote zilizoorodheshwa na shirika la ADOT na wanafunzi wa shule zote mbili amezibeba na ameahidi kushirikiana na shirika kwa hali na mali ili kuendeleza kazi ya Mungu ya kusaidia watoto hasa watoto wenye ulemavu. Vilevile mgeni rasmi aliahidi kushirika na Kamati ya Maendeleo ya Kata kuona namna ya kushirikiana Ili watatue changamoto hizo.

**ZOEZI LA UGAWAJI WA ZAWADI KWA WATOTO WENYE ULEMAVU WA SHULE YA MSINGI CHAMAZI, MSUFINI NA KITUO CHA WATOTO YATIMA.**

Baada ya risala ya mgeni rasmi, zoezi la ugawaji wa zawadi kwa watoto wenye ulemavu lilianza ambapo watoto wenye ulemavu walipewa madaftari, peni, penseli, sabuni, unga, taulo za kike, sukari, mafuta ya kupaka na kupikia, juisi, biskuti, maji nk

*Zoezi la ugawaji wa zawadi kwa watoto wenye ulemavu.*

**MWISHO:**

Mkurugenzi wa Shirika la ADOT aliwashukuru watu wote walioshiriki katika hafla ya siku ya Mtoto wa Afrika. Kulikuwepo na picha ya pamoja na Mkurugenzi wa shirika la ADOT, mgeni rasmi, walimu, sekretariet ya ADOT, wazazi pamoja na watoto wenye ulemavu.

*Picha ya pamoja kati ya watoto wemye ulemavu shule ya msingi chamazi na msufini pamoja na sekretarieti ya ADOT.*